



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. HJD/CS.20/3/VOL.V/12

30 Aprili, 2023

Kwa yeyote anayehusika

Yah: **MABADILIKO YA TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Husika na somo tajwa hapo juu.

2. Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma ilitangaza nafasi za kazi kupitia tangazo lenye Kumb. Na. **HMD/S.20/39/40** la tarehe **20 Aprili, 2023** kwa kadane za Dereva Daraja la II nafasi **09**, Mwandishi Mwendesha Ofisi Daraja la II nafasi **03**, Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II nafasi **03** na Mtendaji wa Mtaa Daraja la III nafasi **20**. Tangazo hilo lilitokana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kupata kibali cha Ajira chenye Kumb. Na. FA.97/228/01"TEMP"/06 cha tarehe 06 Aprili, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu Ajira Mpya.
3. Kutokana na kibali hicho, Ofisi imepokea maelekezo kutoka kwa Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Kanuni Na. 22 (1,2) ya Kanuni za uendeshaji wa shughuli za Sekretarieti ya Ajira inaanisha kutumia Kanzi Data ya watahiniwa waliofaulu usaili na hawakupata nafasi za kazi kwa sababu ya uchache wa nafasi.
4. Kwa kuwa nafasi zilizotangazwa kwa kuzingatia maelekezo ya Katibu wa Sekretarieti ya Ajira, nafasi za maombi ya kazi zitakuwa kama ifuatavyo: -  
**Mtendaji wa Mtaa Daraja la III nafasi 20 na Dereva Daraja la II nafasi 06** kwa kuwa kuna kanzi data ya nafasi tatu za Madereva wenye sifa. Mwandishi Mwendesha Ofisi Daraja la II na Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II hakukutakuwa na nafasi kwa kuwa kuna kanzi data ya usaili uliofanyika tarehe 28 - 30 Aprili, 2023 na kupata wasailiwa wenye sifa.
5. Kwa barua hii, na kuzingatia kuwa hatukufanya usaili kwa kada ya Mtendaji wa Mtaa Daraja la III, nakaribisha maombi kwa kada hiyo pamoja na Dereva Daraja la II na masharti na vigezo vyote vilivyowekwa kwenye tangazo la awali vitabaki kama vilivyo. **Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 03 Mei, 2023.**

7. Naomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.

  
Francis D. Kilawe  
Kny: **MKURUGENZI WA JIJI**  
**DODOMA**

